**SHERIA YA KUWEKA MASHARTI YANAYOSIMAMIA UTOAJI WA HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA, KURAHISISHA UPATIKANAJI WA HAKI NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

**MPANGILIO WA VIFUNGU**


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**IDARA YA MSAADA WA KISHERIA**

3. Uanzishaji wa Idara ya Msaada wa Kisheria.
4. Kazi za Idara.
5. Uteuzi wa Mkurugenzi.
6. Kazi na mamlaka ya Mkurugenzi.
7. Wafanyakazi wa Idara.
8. Kupewa kazi za uratibu.

**SEHEMU YA TATU**
**USAJILI WA WATOAJI WA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA**

9. Ombi kwa ajili ya usajili.
10. Uamuzi kuhusu ombi.
11. Rufaa.
12. Sifa za Msaidizi wa Sheria.

13. Uanzishaji wa daftari.

14. Usitishaji wa cheti.

15. Ombi la mapitio.

16. Kushughulikia sababu za usitishaji.

17. Ufutaji wa cheti.

18. Huduma za msaada wa kisheria za wasaidizi wa sheria.

## SEHEMU YA NNE
## HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA

19. Aina ya msaada wa kisheria.

20. Msaada wa kisheria hautapatikana katika baadhi ya kesi za madai.

21. Viwango kwa ajili ya watoaji wa huduma ya msaada wa kisheria.

22. Ombi kwa ajili ya msaada wa kisheria.

23. Mtu ambaye anaweza kuomba msaada wa kisheria.

24. Sifa za kupata msaada wa kisheria.

25. Kutathmini uwezo.

## SEHEMU YA TANO
## MSAADA WA KISHERIA KATIKA KESI ZA MADAI

26. Msaada wa kisheria katika kesi za madai kwa amri ya Mahakama.

27. Kuwataarifu wahusika wengine wa kesi.

28. Kulipa gharama.

29. Kukata kutoka katika fidia.

30. Kukaza hukumu.

31. Gharama dhidi ya mtu asiyekuwa na uwezo.

32. Dhamana kwa ajili ya gharama.

## SEHEMU YA SITA
## MSAADA WA KISHERIA KATIKA KESI ZA JINAI

33. Msaada wa kisheria kwa amri ya Mahakama.

34. Msaada wa kisheria kwa watoto walio katika vizuizi.

35. Msaada wa kisheria kwa watu waliopo kizuizini.

## SEHEMU YA SABA
## KUTAARIFU MABADILIKO NA KUSITISHA MSAADA WA KISHERIA

36. Kutaarifu mabadiliko kutokana na mazingira.

37. Kusitisha msaada wa kisheria.

38. Usitishaji wa msaada wa kisheria unaofanywa na mtu asiyekuwa na uwezo.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MBALI MBALI

39. Makosa na adhabu.

40. Kanuni.

**SHERIA NAM 13 YA 2018**

**NIMESAINI**

Alshein

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

31 Disemba, 2018

# SHERIA YA KUWEKA MASHARTI YANAYOSIMAMIA UTOAJI WA HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA, KURAHISISHA UPATIKANAJI WA HAKI NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Msaada wa Kisheria, 2018 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri ataitangaza katika Gazeti Rasmi.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Wakili" ina maana kama iliyoelezwa katika sheria ambayo inasimamia usajili na utendaji kazi wa mawakili;

"Idara" maana yake ni Idara iliyoanzishwa chini ya Sheria hii;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Idara aliyeteuliwa chini ya Sheria hii;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"mtu asiyekuwa na uwezo" maana yake ni mtu ambaye hana uwezo wa kulipia huduma za kisheria;

"mwanasheria" maana yake ni mtu ambaye ana shahada ya kwanza ya sheria au inayolingana na hiyo kutoka chuo kikuu kinachotambulika na anatoa huduma za kisheria chini ya mtoaji msaada wa kisheria kwa mujibu wa Sheria hii;

"afisa wa huduma za kisheria" maana yake ni afisa wa umma aliyepewa kazi na Mkurugenzi kuratibu huduma za msaada wa kisheria ndani ya mipaka ya mamlaka ya Serikali ya mtaa husika;

"mtoa msaada wa kisheria" maana yake ni mtu, taasisi au jumuiya iliyosajiliwa kutoa msaada wa kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 9 cha Sheria hii;

"huduma za msaada wa kisheria" inajumuisha utoaji wa ushauri wa kisheria, msaada au uwakilishi wa kisheria, elimu ya kisheria na taarifa kwa watu wasiokuwa na uwezo;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana juu ya msaada wa kisheria;

"msaidizi wa sheria" maana yake ni mtu aliyesajiliwa kutoa huduma za msaada wa kisheria baada ya kukamilisha mafunzo ya lazima katika fani husika ya masomo iliyoidhinishwa au inayotambuliwa na Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Katibu Mkuu" maana yake ni Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana juu ya msaada wa kisheria;

"Daftari" maana yake ni daftari la watoaji wa msaada wa kisheria lililoanzishwa chini ya Sheria hii;

"Mrajis" maana yake ni Mrajis wa Mahakama Kuu;

"Vakili" ina maana kama iliyoelezwa katika sheria ambayo inasimamia usajili na utendaji kazi wa mavakili.

## SEHEMU YA PILI
## IDARA YA MSAADA WA KISHERIA

Uanzishaji wa Idara ya Msaada wa Kisheria.

**3.** Inaanzishwa Idara itakayojulikana kama Idara ya Msaada wa Kisheria ndani ya Wizara ambayo itakuwa na dhamana ya kuratibu, kuendesha na kusimamia utoaji wa msaada wa kisheria.

Kazi za Idara.

**4.**-(1) Idara itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kutoa miongozo ya kisera kwa watoaji wa msaada wa kisheria;

(b) kumshauri Waziri kuhusu sera na mambo mengine muhimu yanayohusu kuimarisha utoaji wa msaada wa kisheria;

(c) kusajili watoaji wa msaada wa kisheria;

(d) kuweka na kutunza Daftari la watoaji msaada wa kisheria, na kuweka kumbukumbu na taarifa zinazohusiana na watoaji wa msaada wa kisheria;

(e) kumtaka mtoa msaada wa kisheria kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa mtu asiyekuwa na uwezo;

(f) kupokea na kujumuisha ripoti za robo mwaka kuhusiana na huduma za msaada wa kisheria kutoka kwa watoaji msaada wa kisheria;

(g) kutayarisha taarifa mbali mbali kuhusu huduma za msaada wa kisheria na mambo mengine kwa ajili ya kuwasilishwa mbele ya Katibu Mkuu;

(h) kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa katika mfumo unaorahisisha upatikanaji wa taarifa hizo na kutoa miongozo kwa ajili ya ushirikiano na mawasiliano baina ya watoaji wa msaada wa kisheria na Serikali;

(i) kuratibu, kufuatilia na kutathmini kazi za watoaji wa msaada wa kisheria na kutoa maelekezo ya jumla kwa ajili ya utekelezaji unaofaa wa programu za msaada wa kisheria katika kiwango kilichowekwa na ubora wa huduma za msaada wa kisheria;

(j) kupokea na kujumuisha taarifa za mwaka za watoaji wa msaada wa kisheria;

(k) kuratibu na kurahisisha utengenezaji na uidhinishaji wa mtaala kwa ajili ya mafunzo ya wasaidizi wa sheria kwa kushauriana na watoaji wa msaada wa kisheria na taasisi za elimu na taasisi za mafunzo;

(l) kushajihisha na kuwezesha utatuzi wa migogoro kupitia njia mbadala za utatuzi wa migogoro;

(m) kuchukua hatua zinazofaa kuimarisha elimu ya sheria na uelewa wa kisheria miongoni mwa jamii na, hususan, kuelimisha makundi maalum kuhusu upatikanaji wa msaada wa kisheria;

(n) kuanzisha na kuendeleza programu kwa ajili ya elimu ya msaada wa kisheria na mafunzo na utoaji vyeti kwa wasaidizi wa sheria;

(o) kupokea na kupeleleza malalamiko na tabia mbaya dhidi ya watoaji wa msaada wa kisheria; na

(p) kutekeleza kazi nyengine zozote kama itakavyoelekezwa na Waziri kuhusu mambo yanayohusiana na Sheria hii.

(2) Katika kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii, Idara itaendeleza kwa kadiri itakavyowezekana, mfumo wa mashauriano na ushirikiano na Mawizara, Taasisi za Serikali, watoaji wa msaada wa kisheria au Taasisi nyengine zozote za umma au za binafsi zilizoanzishwa chini ya sheria nyengine yoyote.

(3) Idara itatekeleza kazi zake kwa haki na kwa uhuru na itatekeleza mamlaka yake na kutekeleza wajibu wake na kutekeleza kazi zake kwa nia njema na bila ya woga, bila ya upendeleo, bila ya kuegemea upande mmoja na bila ya chuki.

Uteuzi wa Mkurugenzi.

**5.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Idara ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atafaa kuwa Mkurugenzi ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza ya sheria kutoka chuo kinachotambulika na Serikali;

(c) ana sifa za kuwa Jaji wa Mahakama Kuu; na

(d) ana kiwango cha juu cha uadilifu.

Kazi na mamlaka ya Mkurugenzi.

**6.**-(1) Mkurugenzi wa Idara, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, atakuwa ni Mkuu wa Idara, na katika wadhifa wake huo, atawajibika kwa Katibu Mkuu katika utendaji wa kila siku.

(2) Mkurugenzi atasimamia utekelezaji wa kazi za Idara zilizoainishwa katika kifungu cha 4 cha Sheria hii.

(3) Mkurugenzi anaweza, kwa idhini ya Katibu Mkuu, kukasimu kwa maandishi, yoyote miongoni mwa mamlaka yake au kazi zake chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote kwa afisa mwengine yeyote au mfanyakazi wa Idara kwa masharti yatakayoainishwa katika hati hiyo ya kukasimu.

Wafanyakazi wa Idara.

**7.** Wafanyakazi wa Idara wataajiriwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Kupewa kazi za uratibu.

**8.** Mkurugenzi, kwa kushauriana na mamlaka ya Serikali ya Mtaa, anaweza kumpa kazi Afisa Sheria wa Halmashauri kuwa afisa wa msaada wa kisheria kwa ajili ya kuratibu ipasavyo huduma za msaada wa kisheria ndani ya mamlaka ya mipaka ya Halmashauri husika.

## SEHEMU YA TATU
## USAJILI WA WATOAJI WA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA

Ombi kwa ajili ya usajili.

**9.**-(1) Mtu, jumuiya au taasisi haitojihusisha katika utoaji wa msaada wa kisheria kwa mtu asiyekuwa na uwezo isipokuwa kama mtu huyo, jumuiya au taasisi hiyo imesajiliwa na Idara kuwa mtoaji msaada wa kisheria.

(2) Mtu anaweza kusajiliwa kuwa mtoaji msaada wa kisheria ikiwa mtu huyo ama ni wakili, mwanasheria, vakili au msaidizi wa sheria.

(3) Jumuiya au taasisi itasajiliwa kuwa mtoaji msaada wa kisheria ikiwa:

(a) imesajiliwa chini ya sheria husika;

(b) utoaji wa huduma za msaada wa kisheria ni moja miongoni mwa kazi zake za msingi;

(c) ina jengo la ofisi na nyenzo za kiofisi;

(d) ina siyo chini ya moja yafuatayo:

(i) mawakili wawili;

(ii) wakili mmoja na mwanasheria mmoja;

(iii) mwanasheria mmoja na vakili wawili au mwanasheria mmoja na wasaidizi wa sheria watatu;

(iv) wakili mmoja na vakili mmoja au wakili mmoja na wasaidizi wa sheria wawili; au

(v) mavakili wawili; na

(e) imethibitishwa na mamlaka iliyoisajili jumuiya au taasisi hiyo kuhusu kumbukumbu zake zinazohusiana na utendaji wake na usimamizi wake wa fedha, na watoaji wa msaada wa kisheria wa Jumuiya au Taasisi hiyo wamesajiliwa chini ya Sheria hii.

(4) Mtu, jumuiya au taasisi inayoomba usajili wa kuwa mtoaji msaada wa kisheria itaonesha:

(a) jina kamili na anuwani ya muombaji;

(b) eneo halisi lililopo jengo la muombaji;

(c) aina ya jumuiya au taasisi na taarifa za usajili wake;

(d) aina ya huduma zinazotolewa;

(e) eneo la kijografia la utoaji wa huduma;

(f) jina na sifa za watendaji wa sheria; na

(g) ama muombaji amekidhi matakwa chini ya kifungu kidogo cha (2) au cha (3) cha kifungu hiki.

Uamuzi kuhusu ombi.

**10.**-(1) Mkurugenzi atazingatia na atafanya maamuzi kuhusiana na ombi la usajili ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupokea ombi hilo.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, katika kufanya maamuzi ya ombi, Mkurugenzi anaweza kusajili au kukataa kusajili mtu au jumuiya au taasisi kuwa mtoaji msaada wa kisheria.

(3) Pale Mkurugenzi anaporidhika kwamba muombaji wa usajili ametimiza matakwa yote yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria hii, atatoa cheti cha usajili ambacho kitampa haki mwenye cheti hicho kutoa huduma za msaada wa kisheria.

(4) Pale Mkurugenzi anakataa kumsajili muombaji kwa ajili ya usajili wa kuwa mtoaji msaada wa kisheria, atatoa sababu za kukataa huko.

Rufaa.

**11.**-(1) Muombaji wa usajili ambaye hajaridhika na maamuzi chini ya kifungu cha 10 anaweza, ndani ya siku kumi na nne (14), kukata rufaa kwa Waziri.

(2) Waziri, ndani ya siku kumi na nne (14) kutoka siku aliyopokea rufaa hiyo, atazingatia na ataamua rufaa hiyo.

(3) Muombaji wa usajili ambaye hajaridhika na maamuzi chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, anaweza kwenda Mahakamani kwa mapitio.

Sifa za Msaidizi wa sheria.

**12.**-(1) Msaidizi wa sheria atatakiwa kuwa na yoyote katika sifa zifuatazo:

(a) shahada ya kwanza katika fani yoyote kutoka katika taasisi inayotambulika na Serikali, isipokuwa shahada ya kwanza ya sheria;

(b) cheti au stashahada kutoka katika taasisi inayotambulika na Serikali; au

(c) cheti chochote cha elimu ya sekondari.

(2) Pamoja na matakwa ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, msaidizi wa sheria atalazimika kupata mafunzo ya lazima kama itakavyoelezwa katika Kanuni.

(3) Bila ya kujali ujumla wa masharti ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, mtu ambaye ameshakuwa msaidizi wa sheria kwa angalau miaka miwili na ameshapata mafunzo chini ya utaratibu uliopo kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, atakuwa na sifa ya kuwa msaidizi wa sheria kwa madhumuni ya Sheria hii.

(4) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki na masharti mengine ya Sheria hii, Mkurugenzi atawatambua na atawasajili wasaidizi wa sheria waliopata mafunzo chini ya mtoaji msaada wa kisheria aliyesajiliwa:

(a) ambaye amekidhi vigezo vya msingi vilivyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki; na

(b) kwa mujibu wa mtaala ulioidhinishwa.

Uanzishaji wa daftari.

**13.**-(1) Kutakuwa na daftari la watoaji msaada wa kisheria ambalo litajumuisha taarifa zilizoelezwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria hii na litajumuisha idadi ya kesi zinazoshughulikiwa na mtoaji msaada wa kisheria katika wakati wowote husika na jambo jengine lolote lililoelezwa na Kanuni.

(2) Mkurugenzi atawezesha daftari, ama kwa kuchapishwa au kwa njia ya elektroniki, kupatikanwa na watu katika jamii katika Vituo vya Polisi, Mahakama, Chuo cha Mafunzo na sehemu nyengine za umma kama itakavyoamuliwa na Waziri.

Usitishaji wa cheti.

**14.**-(1) Mkurugenzi anaweza kusitisha cheti cha usajili wa mtoaji msaada wa kisheria kwa kipindi kilichoainishwa ikiwa mtoaji msaada wa kisheria aliyesajiliwa:

(a) anashindwa kufuata viwango vilivyoelezwa katika Sheria hii;

(b) anakiuka kanuni za utendaji zilizoelezwa chini ya Sheria hii, Kanuni au kanuni za utendaji zilizoelezwa chini ya sheria nyengine yoyote; au

(c) anashindwa kuweka kumbukumbu sahihi za shughuli alizozifanya kwa niaba ya mtu asiyekuwa na uwezo au kutoa msaada wa kisheria, na Mkurugenzi atazingatia kwamba jambo hilo lina athari mbaya kwa maslahi ya mtu asiyekuwa na uwezo kwa jumla au katika kesi yoyote mahsusi.

(2) Kabla ya usitishaji wa cheti, Mkurugenzi atampa mtoaji msaada wa kisheria notisi ya maandishi ya nia yake ya kusitisha, akiainisha sababu za kusitisha huko.

(3) Mtoaji msaada wa kisheria ambaye anapewa notisi chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki anaweza, ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupokea notisi hiyo, kuwasilisha kwa Mkurugenzi taarifa ya maandishi ya kupinga usitishaji huo.

(4) Mkurugenzi atamtaarifu mtoaji msaada wa kisheria kuhusu uamuzi wake ndani ya siku saba (7) baada ya kupokea taarifa ya pingamizi.

(5) Mtoaji msaada wa kisheria ambaye usajili wake unasitishwa atasita kutoa msaada wa kisheria husika.

(6) Muda ulioainishwa ambao umetajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hautazidi miezi sita.

Ombi la mapitio.

**15.**-(1) Mtoaji msaada wa kisheria ambaye usajili wake umesitishwa, anaweza kumuomba Mkurugenzi afanye mapitio ya uamuzi wake ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupokea notisi ya kusitisha.

(2) Mkurugenzi, ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupokea ombi lililoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ataamua na atamtaarifu mtoaji msaada wa kisheria kuhusu uamuzi wake.

Kushughulikia sababu za usitishaji.

**16.** Ikiwa mtoaji msaada wa kisheria:

(a) wakati wa usitishaji, anashughulikia sababu ambazo zilipelekea cheti hicho kusitishwa chini ya aya ya (a), (b) au (c) ya kifungu cha 14(1) cha Sheria hii, Mkurugenzi anaweza kuondoa usitishaji huo; au

(b) ameshindwa kushughulikia, ndani ya kipindi kilichoainishwa, sababu ambazo zilipelekea cheti hicho kusitishwa chini ya aya ya (a), (b) au (c) ya kifungu cha 14(1) cha Sheria hii, Mkurugenzi anaweza kukifuta cheti hicho cha usajili.

Ufutaji wa cheti.

**17.**-(1) Mkurugenzi anaweza kufuta usajili wa mtoaji msaada wa kisheria kutokana na yoyote miongoni mwa sababu zifuatazo, ikiwa:

(a) usajili ulipatikana kimakosa, kwa udanganyifu, kwa ushawishi usiofaa au kwa kutokusema ukweli;

(b) mtoaji msaada wa kisheria:

(i) amesita kuwa na sifa za usajili;

(ii) hatoi huduma, au hajatoa huduma, ambayo alisajiliwa kuitoa kwa kiwango kilichoelezwa;

(iii) Mahakama imemtangaza kuwa amefilisika, hana uwezo wa kulipa madeni au ameshaingia katika makubaliano na wale wanaomdai;

(iv) ameshindwa kufuata moja au zaidi ya moja ya matakwa ya usajili;

(v) ametiwa hatiani kwa kosa linalohusu kutokuwa na uaminifu, udanganyifu au kosa jengine lolote linalohusu tabia mbaya;

(vi) amekiuka mara kwa mara maadili ya kitaaluma; au

(vii) amembagua mtu asiyekuwa na uwezo kwa jinsia, dini, rangi, kabila, ulemavu au mtazamo wa kisiasa.

(2) Kabla ya ufutaji wa cheti, Mkurugenzi atampa mtoaji msaada wa kisheria notisi ya maandishi ya nia yake ya kufuta, akiainisha sababu za kufuta huko.

(3) Mtoaji msaada wa kisheria anayepewa notisi chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki anaweza, ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupokea notisi, kuwasilisha kwa Mkurugenzi taarifa ya kupinga kufutwa huko.

(4) Mkurugenzi atamtaarifu mtoaji msaada wa kisheria kuhusu uamuzi wake ndani ya siku saba (7) baada ya kupokea taarifa ya pingamizi.

(5) Mtoaji msaada wa kisheria ambaye usajili wake umefutwa, atasita kutoa msaada wa kisheria husika.

(6) Mtoaji msaada wa kisheria ambaye hakuridhika na uamuzi wa Mkurugenzi wa kufuta cheti, anaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku kumi na nne (14) kutoka tarehe ya kupokea ufutaji huo.

(7) Waziri, ndani ya siku ishirini na moja (21) kutoka siku ya kupokea rufaa, ataiamua rufaa hiyo.

Huduma za msaada wa kisheria za wasaidizi wa sheria.

**18.**-(1) Msaidizi wa sheria hatajihusisha katika shughuli ambayo imewekwa kwa ajili ya mawakili na mavakili tu chini ya sheria yoyote.

(2) Msaidizi wa sheria hatatoza ada yoyote kutoka kwa mtu asiyekuwa na uwezo kwa ajili ya utoaji wa msaada wa kisheria chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA NNE
## HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA

Aina ya msaada wa kisheria.

**19.**-(1) Msaada wa kisheria utajumuisha:

(a) ushauri wa kisheria;

(b) msaada wa kisheria;

(c) uwakilishi katika Mahakama au kwenye Baraza la Maamuzi; na

(d) elimu ya kisheria na uhamasishaji.

(2) Watoaji msaada wa kisheria watatoa huduma za msaada wa kisheria katika:

(a) mambo ya madai;

(b) mambo ya jinai;

(c) mambo yanayohusu watoto;

(d) mambo ya Katiba kuhusu haki za msingi za mtu binafsi;

(e) kesi za madai ya kijamii; au

(f) aina nyengine yoyote ya kesi au aina ya sheria ambayo Idara inaweza kuidhinisha.

(3) Ushauri, msaada au uwakilishi kupitia msaada wa kisheria hautaathiri uhusiano baina ya haki za wakili na mteja au fursa yoyote inayotokana na uhusiano huo.

(4) Bila ya kuathiri mamlaka ya Mahakama Kuu chini ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai na kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, aina ya msaada wa kisheria unaotolewa kwa mtu asiyekuwa na uwezo katika kesi yoyote mahsusi itakuwa kwa hiyari ya mtoaji msaada wa kisheria, akizingatia mahitaji ya mtu husika na rasilimali zilizopo kwa mtoaji msaada wa kisheria.

Msaada wa kisheria hautapatikana katika baadhi ya kesi za madai.

**20.** Watoaji msaada wa kisheria hawatatoa huduma za msaada wa kisheria kuhusiana na kesi za madai zifuatazo:

(a) kwa kampuni, shirika, taasisi ya amana, taasisi ya umma, jumuiya ya kiraia, jumuiya isiyokuwa ya Serikali au mtu mwengine wa kisheria;

(b) katika mambo yanayohusu kodi;

(c) katika mambo yanayohusu ulipaji wa madeni; na

(d) katika kesi za ufilisi na kutokuweza kulipa madeni.

Viwango kwa ajili ya watoaji wa huduma ya msaada wa kisheria.

**21.**-(1) Mtoaji msaada wa kisheria atahakikisha kwamba watu wasiokuwa na uwezo wanapewa huduma za msaada wa kisheria za hali ya juu, zenye ubora na kwa wakati ambazo zinajumuisha:

(a) ukarimu, huduma zenye kupatikanwa na zinazofaa;

(b) mazingira yanayofaa kwa ajili ya usiri;

(c) ushughulikiaji wa watoto kitaalamu na kwa unyeti, watu wenye ulemavu, wazee, au watu wa makundi maalum;

(d) utoaji wa taarifa kuhusu upatikanaji na aina ya huduma zinazotolewa na taarifa nyengine yoyote; na

(e) kutekeleza kwa mujibu wa maelekezo ya mtu asiyekuwa na uwezo, au ikiwa haiwezekani, kwa maslahi bora ya mtu asiyekuwa na uwezo.

(2) Mtoaji msaada wa kisheria chini ya Sheria hii atatakiwa kufuata kanuni zozote au kanuni za utendaji zinazoongoza taaluma ambayo mtoaji huyo wa msaada wa kisheria anahusika nayo na haki zake, wajibu, dhamana au majukumu kama mhusika wa taaluma hiyo hayataathiriwa kwa masharti ya Sheria hii kwa namna yoyote ile.

(3) Waziri, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, atatunga kanuni za utendaji kwa ajili ya watoaji msaada wa kisheria.

(4) Kanuni za utendaji zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, zitaweka masharti kwa ajili ya:

(a) kulinda haki na maslahi ya mtu asiyekuwa na uwezo;

(b) wajibu kwa mtu asiyekuwa na uwezo;

(c) mgongano wa maslahi;

(d) kulinda usiri;

(e) katika mazingira ya wanataaluma, wajibu wa kulinda viwango vya maadili vilivyoelezwa vya taaluma zao husika;

(f) kutokufanya ubaguzi;

(g) uadilifu na mwenendo wa maadili; na

(h) jambo jengine lolote linalohusiana na msaada wa kisheria.

Ombi kwa ajili ya msaada wa kisheria.

**22.**-(1) Mtu asiyekuwa na uwezo ambaye anakusudia kupokea msaada wa kisheria anaweza kuwasiliana na mtoaji msaada wa kisheria yeyote na kuomba huduma za msaada wa kisheria.

(2) Mtoaji msaada wa kisheria, baada ya kupokea ombi kwa ajili ya msaada wa kisheria, atazingatia ombi hilo na:

(a) atalikubali ombi hilo na kutoa msaada wa kisheria kwa muombaji, ikiwa mtoaji msaada wa kisheria anaridhika kwamba:

(i) muombaji ana sifa za kupewa msaada wa kisheria; na

(ii) mtoaji msaada wa kisheria ana, katika wakati huo, rasilimali za kutosha kutoa msaada wa kisheria unaohitajika; au

(b) ikiwa mtoaji msaada wa kisheria hajaridhika kwamba muombaji ana sifa za kupewa msaada wa kisheria, atakataa ombi hilo.

(3) Mtoaji msaada wa kisheria anaweza wakati wowote kuzingatia upya uamuzi wowote alioufanya chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki kuhusu kustahiki kwa mtu yeyote kupokea msaada wa kisheria.

Mtu ambaye anaweza kuomba msaada wa kisheria.

**23.** Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 22 cha Sheria hii, ombi kwa ajili ya msaada wa kisheria linaweza kufanywa na:

(a) mtu asiyekuwa na uwezo;

(b) mtu mwengine yeyote aliyeidhinishwa na mtu asiyekuwa na uwezo; au

(c) mtu yeyote au taasisi yoyote kwa niaba ya mtu asiyekuwa na uwezo pale endapo idhini ya mtu asiyekuwa na uwezo haiwezi kupatikana kwa wakati.

**Sifa za kupata msaada wa kisheria.**

**24.** Mtu anastahiki kupokea huduma za msaada wa kisheria ikiwa mtu huyo ni mtu asiyekuwa na uwezo na kwa maoni ya mtoaji msaada wa kisheria:

(a) hana uwezo wa kutosha kulipia huduma za wakili au vakili kwa fedha zake yeye mwenyewe;

(b) ana sababu za msingi za kuanzisha, kuendeleza, au kutetea jambo ambalo kwa jambo hilo anaomba msaada wa kisheria, au jambo hilo lina maslahi ya umma;

(c) dai ambalo msaada wa kisheria unaombwa lina uwezekano wa kufanikiwa;

(d) mtu asiyekuwa na uwezo anahitaji au atanufaika kutokana na msaada wa kisheria;

(e) kumkatalia msaada wa kisheria kutapelekea kukosekana haki kwa mtu asiyekuwa na uwezo; au

(f) kuna sababu nyengine yoyote ya msingi inayohalalisha kutolewa kwa msaada wa kisheria.

**Kutathmini uwezo.**

**25.** Katika kutathmini uwezo wa mtu yeyote kwa madhumuni ya kuamua ama mtu huyo anastahiki msaada wa kisheria, mtoaji msaada wa kisheria atazingatia kipato na mali za mtu asiyekuwa na uwezo.

## SEHEMU YA TANO
## MSAADA WA KISHERIA KATIKA KESI ZA MADAI

**Msaada wa kisheria katika kesi za madai kwa amri ya Mahakama.**

**26.** Endapo katika kesi za madai, kuhusiana na mambo ambayo hayajakatazwa chini ya kifungu cha 20, inaonekana na Jaji anayeongoza Mahakama au Hakimu kwamba:

(a) kwa maslahi ya upatikanaji wa haki, mtu anapaswa kupewa msaada wa kisheria; na

(b) mtu hana uwezo wa kutosha wa kumuwezesha kupata huduma za kisheria,

Jaji anayeongoza Mahakama au Hakimu, atawezesha mtu huyo kupata msaada wa kisheria.

Kuwataarifu wahusika wengine wa kesi.

**27.**-(1) Pale mhusika wa kesi ya madai anapewa msaada wa kisheria, mtoaji msaada wa kisheria atamtaarifu mara moja kila mhusika mwengine wa kesi katika kesi hiyo na Mahakama, kuhusu jambo hilo.

(2) Pale mtu mwengine yeyote baadae anakuwa mhusika wa kesi katika kesi hiyo, mtoaji msaada wa kisheria atamtaarifu mhusika mpya wa kesi.

(3) Pale mtoaji msaada wa kisheria anajiondoa au anaondolewa na mtu asiyekuwa na uwezo, mtoaji msaada wa kisheria atawaarifu mara moja wahusika wote wa kesi katika kesi hiyo na Mahakama, kuhusu jambo hilo.

Kulipa gharama.

**28.**-(1) Endapo mtu asiyekuwa na uwezo ametakiwa alipwe gharama katika kesi yoyote, mtu huyo asiyekuwa na uwezo atastahiki kulipwa gharama hizo.

(2) Mtoaji msaada wa kisheria anaweza kuwa na haki ya kukata kutoka katika malipo, gharama ambazo alizoziingia kuhusiana na kesi hiyo.

Kukata kutoka katika fidia.

**29.** Mtoaji msaada wa kisheria anaweza, katika utoaji wa msaada wa kisheria, kukata kutoka katika:

(a) fidia ambayo imeruhusiwa na Mahakama kulipwa kwa mtu asiyekuwa na uwezo; au

(b) viwango vinavyostahiki kulipwa kwa mtu asiyekuwa na uwezo kwa mujibu wa makubaliano yaliyofanywa kwa msaada uliotolewa chini ya Sheria hii, kiwango kisichozidi asilimia tano (5%) ya fidia au viwango vilivyolipwa kwa mujibu wa makubaliano, kama hali itakavyokuwa.

Kukaza hukumu.

**30.** Mtoaji msaada wa kisheria atachukua hatua za lazima kukaza hukumu au makubaliano yoyote ili kulipwa mapato ya kesi.

Gharama dhidi ya mtu asiyekuwa na uwezo.

**31.** Pale mtu asiyekuwa na uwezo anapokea msaada wa kisheria kwa ajili ya kesi ya madai na anashindwa kesi hiyo, Mahakama haitatoa amri ya kutoza gharama dhidi ya mtu asiyekuwa na uwezo.

Dhamana kwa ajili ya gharama.

**32.** Bila ya kujali masharti ya sheria yoyote, mtu asiyekuwa na uwezo hatotakiwa kutoa dhamana kwa ajili ya gharama wakati wa usikilizaji wa kesi au rufaa.

## SEHEMU YA SITA
## MSAADA WA KISHERIA KATIKA KESI ZA JINAI

Msaada wa kisheria kwa amri ya Mahakama.

**33.**-(1) Mahakama katika kesi za jinai inaweza, isipokuwa katika makosa ya uhujumu uchumi au kesi za kujamiiana, kesi za dawa za kulevya na kesi za rushwa, kuthibitisha kwamba mtu apewe uwakilishi wa kisheria kwa gharama za Serikali, ikiwa Mahakama imezingatia:

(a) kutokuwa na uwezo wa kutosha kwa mshtakiwa kupata huduma za kisheria;

(b) maslahi ya upatikanaji wa haki katika matayarisho na kuleta utetezi au rufaa;

(c) aina na uzito wa shtaka ambalo mshtakiwa anashtakiwa nalo au shtaka ambalo mshtakiwa ametiwa hatiani;

(d) ama uwakilishi mwengine wowote wa kisheria kwa gharama za Serikali unapatikana au umeshatolewa;

(e) ama mshtakiwa ameshaomba uwakilishi wa kisheria na hajapokea jibu lolote kutokana na ombi hilo ndani ya muda unaostahiki; au

(f) sababu nyengine yoyote ambayo kwa maoni ya Mahakama inapaswa kuzingatiwa.

(2) Baada ya uthibitisho huo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mrajis au Hakimu dhamana kwa kushauriana na Mrajis, atampangia mshtakiwa huyo wakili au vakili kwa madhumuni ya matayarisho na kuleta utetezi wake au rufaa, kama hali itakavyokuwa.

(3) Jaji Mkuu, kwa kanuni zitakazochapishwa katika Gazeti la Serikali, ataamua malipo ya wakili au vakili aliyepangiwa mshtakiwa chini ya masharti ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki.

Msaada wa kisheria kwa watoto walio katika vizuizi.

**34.** Endapo mtu anapewa dhamana ya jukumu la kusimamia ustawi wa mtoto, katika utekelezaji wa majukumu yake anamshughulikia mtoto ambaye anakinzana na sheria, atawezesha mtoto huyo kupata msaada wa kisheria haraka.

Msaada wa kisheria kwa watu waliopo kizuizini.

**35.**-(1) Jeshi la Polisi, Chuo cha Mafunzo au nyumba ya mahabusu ya watoto itatengeneza utaratibu kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa watoaji msaada wa kisheria kwa watu wanaoshtakiwa au waliotiwa hatiani waliopo kizuizini.

(2) Afisa dhamana wa Chuo cha Mafunzo, kituo cha Polisi, nyumba ya mahabusu ya watoto au pahala pengine pa hifadhi ya kisheria atahakikisha kwamba mtu aliyopo kizuizini, anajulishwa, katika lugha ambayo mtu huyo anaifahamu, kuhusu upatikanaji wa msaada wa kisheria wakati anawekwa kizuizini na anaulizwa kama anapenda kupewa msaada wa kisheria.

## SEHEMU YA SABA
## KUTAARIFU MABADILIKO NA KUSITISHA MSAADA WA KISHERIA

Kutaarifu mabadiliko kutokana na mazingira.

**36.**-(1) Mtu asiyekuwa na uwezo au mtu anayemuwakilisha mtu asiyekuwa na uwezo atamuarifu mtoaji msaada wa kisheria kuhusu:

(a) ongezeko lolote la kipato chake au mtaji unaoweza kuhaulishwa kwa kiwango ambacho kinaweza kuathiri kustahiki kwake kupata msaada wa kisheria; na

(b) mabadiliko yoyote ya anuwani yake.

(2) Ikiwa mtu asiyekuwa na uwezo au mtu anayemuwakilisha mtu asiyekuwa na uwezo anakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtoaji msaada wa kisheria anaweza kusitisha huduma ya msaada wa kisheria.

Kusitisha msaada wa kisheria.

**37.**-(1) Mtoaji msaada wa kisheria anaweza, wakati wowote, kusitisha huduma ya msaada wa kisheria inayotolewa na mtoaji msaada wa kisheria huyo kwa mtu asiyekuwa na uwezo kwa mujibu wa Sheria hii kwa sababu yoyote kati ya hizi zifuatazo:

(a) pale mtu asiyekuwa na uwezo hatoi ushirikiano kwa mtoa msaada wa kisheria;

(b) pale mtu asiyekuwa na uwezo anashindwa kufika, bila ya sababu ya msingi wakati anapotakiwa kufanya hivyo na mtoaji msaada wa kisheria au na Mahakama;

(c) pale mtu asiyekuwa na uwezo anatoa taarifa za uongo kwa mtoaji msaada wa kisheria;

(d) pale mtoaji msaada wa kisheria ana uthibitisho kwamba mtu asiyekuwa na uwezo amelipeleka suala lake ama kwa mtoaji msaada wa kisheria mwengine au kwa wakili binafsi;

(e) pale mtu asiyekuwa na uwezo anasita kuwa hana uwezo; au

(f) kwa sababu nyengine yoyote ya msingi.

(2) Mtoaji msaada wa kisheria hatositisha huduma ya msaada wa kisheria anayoitoa kwa mtu asiyekuwa na uwezo chini ya Sheria hii, isipokuwa kama mtoaji msaada wa kisheria amempa taarifa ya siku thelathini (30) mtu asiyekuwa na uwezo na ametoa fursa kwa mtu huyo asiyekuwa na uwezo kuonesha sababu kwa nini mtoaji msaada wa kisheria asisitishe huduma hiyo.

(3) Endapo jambo lipo Mahakamani au katika Baraza la Maamuzi, mtoaji msaada wa kisheria ataitaarifu Mahakama au Baraza la Maamuzi kuhusu usitishaji huo.

Usitishaji wa msaada wa kisheria unaofanywa na mtu asiyekuwa na uwezo.

**38.** Bila ya kujali kitu chochote kilicho kinyume na Sheria hii, mtu asiyekuwa na uwezo anaweza wakati wowote kusitisha huduma ya msaada wa kisheria inayotolewa kwake.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

Makosa na adhabu.

**39.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anafanya kazi kama mtoaji msaada wa kisheria bila ya cheti cha usajili kinachotolewa na Mkurugenzi;

(b) anafanya kazi kama mtoaji msaada wa kisheria wakati cheti cha usajili kimesitishwa; au

(c) kwa makusudi, anamzuia mtu aliyopo katika kizuizi halali asiombe msaada wa kisheria,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili na Elfu Hamsini lakini isiyozidi Shilingi Laki Tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu lakini kisichozidi miezi sita.

Kanuni.

**40.**-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kujali ujumla wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kanuni zitakazotungwa chini ya kifungu hiki zinaweza kuweka masharti kwa ajili ya:

(a) taratibu, vigezo na masharti ya usajili wa watoaji msaada wa kisheria na wasaidizi wa sheria;

(b) kumbukumbu zitakazowekwa na watoaji msaada wa kisheria kuhusiana na kazi za msaada wa kisheria na taarifa zitakazowasilishwa kwa Mkurugenzi;

(c) taratibu za rufaa chini ya Sheria hii; na

(d) jambo jengine lolote ambalo linahitaji kuelezwa chini ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar tarehe 28 Novemba, 2018.

.......................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi***
***Zanzibar.***